

**KUBADILISHIWA CHEO/KAZI WALIMU BAADA YA  
KUJIENDELEZA KITAALUMA NA KITAALAMU**

***Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma***

Ndugu msomaji wiki iliyopita tulipata fursa ya kuangalia juu ya kuthibitishwa kazini walimu ambapo tuliona kuwa kuthibitishwa kazini ni haki ya mwalimu na kwamba mwalimu hupata fursa ya kupata haki zake kama vile mafao ya kustaafu au madaraka katika utumishi wake. Leo tutaangalia kubadilishwa cheo kwa mwalimu baada ya kujiendeleza. Kwa mujibu wa Sheria Na. 8 ya 2002 kifungu 6 (4) na Kanuni 6 (h) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2003, Idara ya Utumishi wa Walimu ni Mamlaka ya Kubadilishia Walimu vyeo/Kazi.

Kubadilishia cheo/kazi ni kumtoa mwalimu kwenye kada anayotumikia na kumuingiza kwenye kada nyingine ya juu yake baada ya kujiendeleza **Kitaaluma** na **Kitaalam**.

Walimu kutoka daraja la IIIC na IIIB hubadilishiwa daraja la kusomea na kupewa daraja la IIIA baada ya kufaulu mtihani wa Kidato cha IV na mafunzo ya Ualimu daraja la IIIA.

Hivi sasa walimu wa daraja la IIIC/IIIB hufanya mtihani wa ualimu wa daraja la IIIA baada ya kupitia Mafunzo ya Ualimu kazini (MUKA) yanayoratibiwa na Wizara Elimu na Mafunzo ya Ufundi bila kufanya mtihani wa Kidato cha IV. Kwa walimu wa daraja la IIIA kwenda

Afisaelmu Msaidizi, Mwalimu hana budi kujiendeleza na kufaulu mtihani wa Kidato cha VI kisha kufuzu mafunzo ya Stashahada ya Ualimu.

Katika kundi hili wapo pia walimu wa daraja la IIIA ambao husomea Stashahada za Uongozi Bagamoyo, Stashahada ya Elimu Maalumu katika Chuo cha Ualimu Patandi na Stashahada ya Elimu ya Watu Wazima katika chuo cha Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Dar es Salaam.

Walimu wenye Stashahada hujiendeleza na kuwa Maafisa Elimu baada ya kuhitimu Shahada za Ualimu au Shahada nyingine yoyote lenye ualimu. Kwa walimu wanaojiendeleza kwa kusoma Shahada zisizo na ualimu ni lazima asome Stashahada ya Uzamili ya Ualimu (Post Graduate diploma in Education) ili aweze kutambuliwa kama mwenye shahada yenye ualimu.

Aidha zoezi la kubadilishia walimu vyeo/kazi na daraja la kusomea ni kwa mujibu wa Waraka Na. 11 wa mwaka 2002 na nyongeza I, II na III unaofafanua Miundo ya Utumishi ya kada zilizo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

## **UTARATIBU WA KUFUATA ILI MWALIMU AWEZE KUBADILISHIWA CHEO/KAZI AU DARAJA LA KUSOMEA.**

Baada ya kusoma na kuhitimu mafunzo husika kufaulu mitihani iliyopo kisheria, mwalimu hupaswa kufuata taratibu zifuatazo ili abadilishiwe cheo/kazi au daraja la kusomea.

- Kuomba kubadilishiwa cheo/kazi au daraja la kusomea kwa Mamlaka husika kwa Naibu Katibu, Idara ya Utumishi wa Walimu na kuambatisha vyeti vyake.
- Maombi lazima yapitie kwa mwajiri wa mwalimu husika
- Idara ya Utumishi wa Walimu Makao Makuu huhakiki maombi ya walimu na vyeti vilivyoambatishwa ili kujiridhirisha na maombi hayo
- Maombi hupitishwa rasmi na kikao cha kisheria cha Idara ambacho hufanyika mara 4 kwa mwaka na kuridhia/ kuidhinisha mabadiliko hayo kiutumishi.
- Mwalimu hupewa barua kulingana na kada sahihi.

## **MAMBO MUHIMU YA UFAHAMU KATIKA KUBADILISHA VYEO/KAZI NA DARAJA LA KUSOMEA.**

- Utumishi wa awali wa mtumishi aliyekiendeleza na kupata sifa mpya unaendelea kwamba mtumishi haajiriwi upya kama baadhi ya Waajiri wanavyoelewa kwa kuwataka watumishi hao kujaza Mikataba mipya ya ajira.

- Kubadilishaiwa cheo/kazi (recategorization) ni tofauti na kupanda cheo (promotion) na sio lazima ibadilishe mshahara binafsi wa mwalimu mathalani kwa kuongezeka.
- Mwalimu anapobadilishiwa cheo/kazi hutolewa kwenye kada aliyomo na kuingizwa kwenye kada anayotakiwa kuingizwa kwa sifa aliyopata baada ya kujiendeleza, na kupewa ngazi ya mshahara ya kuingilia (ya chini kabisa) katika kada mpya bila kuathiri mshahara wake anaoupata.
- Wanaoweza kufaidika ni wale tu ambao ngazi zao za mishahara ya awali ni ndogo zaidi kuliko zile za kada mpya. Mfano Mwalimu anayepata mshahara wa ngazi ya TGTS C akajiendeleza na kupata shahada hivyo kuingizwa kwenye kada ya Afisaelimu kwa ngazi ya mshahara ya **TGTS D** ambayo ndiyo ya chini zaidi katika kada ya maafisaelimu. Hapo mwalimu hupaswa kumwandikia mwajiri ili kumjulisha mabadiliko ya mshahara wake kisheria ili urekebishwe.
- Hakuna sheria inayotaja mwalimu kupandishwa cheo baada ya kujiendeleza. Mwalimu atapanda cheo kwa utaratibu uliopo.
- Hakuna nyongeza za mshahara zitakazotolewa kwa mwalimu anayekiendeleza kwa kiwango cha kada ya **Mwalimu, Afisaelimu Msaidizi** na **Afisaelimu**, Mwalimu ataomba nyongeza mbili (2) za mshahara kwa mwajiri wake iwapo atahitimu Shahada ya uzamili.

**Ikiwa una maoni, ushauri au maswali tafadhali tuandikie:-**

**Katiibu,**

**Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma,**

**S.L.P. 9143,**

**Dar es Salaam.**